# Hedaya ni nini?

---

Hedaya ni neno linalomaanisha zawadi. Ni zawadi inayotolewa kuonyesha shukrani,  au kuridhishwa kwa wema Fulani uliofanyiwa au  kwa uzuri wake.

Katika biblia Neno hilo tunaliona katika vifungu vifuatavyo;

> *Zaburi 68:28 "Ee Mungu, uziamuru nguvu zako; Ee Mungu, uwe hodari uliyetufanyia makuu.*
>
> *29 Kwa ajili ya hekalu lako Yerusalemu Wafalme watakuletea hedaya".*

> *Zaburi 76:11 "Wekeni nadhiri, mkaziondoe Kwa Bwana, Mungu wenu. Wote wanaomzunguka wamletee hedaya, Yeye astahiliye kuogopwa".*

> *Isaya 18:7 “Wakati huo Bwana wa majeshi ataletewa hedaya na watu warefu, laini; Watu watishao tangu mwanzo wao hata sasa; Taifa la wenye nguvu, wakanyagao watu, Ambao mito inakata nchi yao; mpaka mahali pa jina la Bwana wa majeshi,mlima Sayuni”.*

Hata sisi leo hii kila mmojawetu analojukumu la kumpelekea Mungu wetu hedaya,

Na tunampelekea kwa njia mbili:

Njia ya kwanza: ni kwa sifa za midomo yetu: Yaani kumsifu na kumwabudu, na kumpa shukrani kwa vinywa vyetu kwa wema wake wote anaotutuendea, na kwa ukuu wake wote alionao ulimwenguni kote.

Njia ya pili: Ni kwa Kumtolea sadaka: Unapotoa sadaka( yaani fedha, mali n.k.), ni unaonyesha shukrani kwa Mungu, kwa kile alichokufanyia, unaonyesha shukrani kwa neema aliyokupa ya uhai, na kila kitu.

Hivyo huo ni wajibu wa kila mmojawetu. Na hiyo ndio tafsiri ya Hedaya kibiblia.

Shalom.

jiunge na channel yetu Kwa kubofya hapa >> WHATSAPP

Tazama maana nyingine za maneno chini;

Tafadhali washirikishe na wengine habari hizi njema, na pia kama utapenda tuwe tunakutumia mafundisho ya Neno la Mungu ya mara kwa mara kwa njia ya email yako au Whatsapp basi tutumie ujumbe kwenye namba hii +255 789001312 / 0693036618.

Mada Nyinginezo:

> *Mkatale ni nini katika biblia? (Matendo 16:24)*

> *Daawa ni nini kama tunavyosoma katika biblia?*

> *UHARIBIFU HAUNA KIFUNIKO.*

> *TAFUTA KUIFANYA KAZI YA MUNGU KWA HUDUMA MUNGU ALIYOIWEKA NDANI YAKO.*

> *NA MTU MMOJA AKAVUTA UPINDE KWA KUBAHATISHA, AKAMPIGA MFALME*

> *Amin, nawaambia, Kizazi hiki hakitapita..*

> *CHUKIZO LA UHARIBIFU*

Rudi Nyumbani:

Share on:
WhatsApp